UCHAMBUZI WA CHOZI LA HERI

SURA 1

MANDHARI: mabaki ya jumba la Ridhaa lililobaki baada ya kuchomwa wakati wa vurugu za baada ya uchaguzi

Mandhari haya ya mabaki ya nyumba ya Ridhaa yametumika kujenga maudhui ya dhuluma kwa vile Ridhaa alipoteza nyumba na familia

Msitu wa heri

- **Wahusika**: Ridhaa
- **Terry** : mkewe ridhaa
- **Tila** : bintiye ridhaa
- **Mwangeka** ; mwanawe Ridhaa anatajwa
- **Mzee Mwimo Msumbili** ; babake Ridhaa
- **Lily Nyamvula** : mkewe Mwangeka
- **BECKY** :mjukuu wa Ridhaa na mwanawe Mwangeka
- **Mzee Kedi** :jiraniye Ridhaa .aliyehusika kuchoma nyumba ya Ridhaa
- **Mzee Shamu**:uk.9,jiraniye Ridhaa

Matukio :/VITUSHI

- Ridhaa anachomewa nyumba katika fujo za baada ya uchaguzi kwa vile ni mgeni
- Anapoteza nyumba zake katika mtaa wa Tononokeni

- Usuli/historia ya ridhaa inarejewa katika hadithi:
- Jinsi walihamia msitu wa heri na kupuuzwa kwa ugeni wao

Maudhui : uhasama wa baada ya uchaguzi unaleta maafa na uharibifu

- Taasubi ya kiume.;mwanaume hapaswi kulia
- Ukatili
- Ufisadi;kutoa hongo ili majumba yasibomolewe
- Ukiukaji wa haki: haki ya kiushi inakiukwaa ,tila becky na nyumvula wauawa

Ridhaa anapoteza haki ya kumiliki mali.nyumba inachomwa

Mbinu za Sanaa:

- Mbinu rejeshi
- **Jazanda/sitiari** uk.5.mtoto wa miaka hamsini
- **Kejeli** uk.5 .mtoto wa miaka hamsini
- **Taashira**: kilio cha bundi na kereng’ende kuashiria hatari na maafa ya ridhaa kupoteza mke wana na nyumba
- **Taswira** .mabaki ya nyumba ya ridhaa iliyochomwa

Kinaya :Mzee Kedi anasaidiwa na ridhaa kuelimisha wapwaze 2.UK11

JB KIPSANG

Sura 2.

Mandhari: Kambi ya wakimbizi/ msitu wa mamba.

Wahusika: Kaizari,
Lime,
Mwanaheri
Tetei
Mwekevu Tendakazi
Bi. Shali
Mwanzi
Hitman
Papa
Kiboko
Tulia
Selume
Mzee Kaumu
Bw.Kute

Matukio:
- Vurugu za baada ya uchaguzi wa Mwekevu.
- Ukimbizi – wakimbizi wako kambini. Kaizari, Mwanaheri na Lime(mabinti wa kaizari)
- Ahadi za uongo zinakasirisha hitman.
- Kaizari na wakimbizi wanaishi kambi ya wambizi/ msitu wa mamba.
- Kazari anasimulia shida walizopata wakati wa fujo na ukimbizi.

Maudhui:
- Matatizo yanayokumba wakimbizi
- Ufisadi
- Elimu – kama chombo cha kuinua maisha kiuchumi na kuzindua.

Lugha/ tamathali za usemi

- Methali, tashihisi, mbinu rejeshi, kinaya, tasfida.ritifaa ?(uk.4 ,5.7)

Sura 3.

Mandhari: - uwanja wa kimataifa wa ndege wa **Rubia.**

Matukio:
- Ridhaa amefika kumpokea Mwangeka(mwanawe)
- Ridhaa anakumbuka shida alizopata akiwa msitu wa mamba.

JB KIPSANG

- Anakumbuka mazungumzo yake na Tila (bintiye) kuhusu uongozi.hadithi ndani ya hadithi .uk .38-44.uongozi unaangaziwa .
- Anakumbuka maisha ya Mwangeka – namna walikuwa na mzaha (kuigiza maombolezi ya Dede – ndugu yake). Namna walivyoadhibiwa na Ridhaa.
- Maisha ya kitaaluma ya Mwangeka – mhandisi, jeshi la wanamaji.
- Ufisadi - Kuuziwa viwanja vya ujenzi kiufisadi.

Maudhui: - ***ufisadi*** – kuuza viwanja kitapeli
- ***Uozo*** – kuchota mafuta/Uozo wa wizi wa mafuta barabarani.
-
- ***Uwajibikaji*** – makaa alijaribu kuokoa wanaoiba mafuta.
- ***Ridhaa*** – anashauri Mwangeka awe makini achunguze mashamba asitapeliwe.
- ***Tamaa*** – wizi wa mafuta
- ***Elimu*** – chombo cha riziki
  - Chombo cha mabadiliko Uk.39

Wahusika: - Tila
- Ridhaa
- Mwangeka
- Mwalimu Meli

Lugha: - jazanda
- Kinaya
- Tashsihi
- Chuku
- Kuchanganya msimbo
- Methali
- Uzungumzi nafsi

<u>Sura 4.</u>

Mandhari: - nyumbani mwa Mwangeka,karibu na klidimbwi cha kuogelea .
Jumba hili lilimletea mwangeka huzuni na kumbukizi za mkewe (lily Nyamvula)hivyo alihamia kwingine kuanza maisha mapya
- Karibu na ufuo.

Matukio: - Mwangeka anahuzunikia kupoteza mkewe, Lily Nyamvula na mwanawe.
- Anashangazwa na hali ya Ridhaa kutoondoa mabaki ya nyumba.

JB KIPSANG

- Mwangeka anahamia kwingine kuishi maisha mapya.
- Ridhaa anasimulia jinsi alipoteza nyumba na majumba katika mtaa wa TONONOKENI
- Watu wanaiba mafuta kisha wanaungua.UK.54

Maudhui: Tamaa – kuiba mafuta kisha kuungua.

Uwajibikaji:
- makaa kujaribu kuokoa wanaochomeka
- Ufisadi – utapeli katika uuzaji wa ardhi.

Lugha:
- Tashihisi
- Chuku
- Kuchanganya ndimi
- Uzungumzi nafsi
- Tashbihi

Sura 5.

Mandhari: - msitu wa mamba/KAMBI YA WAKIMBIZI

Matukio: - wakimbizi wanakataa kurudi kwao kutoka msituni
- Bw. Kangata na familia waliofanya msitu makaazi yao.
- Waliishi kwa tajiri Kiriri
- Familia ya Kangata na Ndarine (mke) ni Lucia, Akelo, Lunga.
- Kiriri (mwajiri wa Kangata) walikuwa wakiishi mtaa wa Matunda.
- Kiriri anaachwa na Annette(mkewe) aliyehamia ng'ambo na wanawe.
- Dada zake lunga kiriri – Lucia Kiriri – Kangata ,Akello, Kiriri – Kangata wameolewa.
- Lucia anaolewa na waombwe naye Akelo anaolewa nas dereva wa lori wa Kongo(Kaango)
- Lunga anaishi katika shamba la wazazi (msitu wa mamba)
- Lunga anafutwa kazi katika shirika la maghala na fanaka – alipopinga kuuziwa wananchi mahindi ya sumu.
- Wakaazi wa msitu wa mamba wanaohamishwa hadi mlima wa simba, msitu unabaki tasa.

Wahusika:- Lunga
- Kiriri
- Kangata
- Akello
- Kaango
- Lucia
- Ndarine
- Annete

JB KIPSANG

- Kimondo

Maudhui: - Uongozi mbaya – kuuzia watu mahindi yenye sumu.
- Ukatili – waandamanaji kuvamiwa, kuhamisha watu msituni kikatili
- Uharibifu wa mazingira
- Usaliti –Lunga anafanya kazi vyema, anasalitiwa kwa kufutwa kazi.
- Ukoloni mamboleo – mzungu anamiliki shamba ambamo Kimundo wanaishi.

LUGHA/TAMATHALI:hotuba :uk.68-69 .lugha shuleni .utunzi wa mazingira barua .72.kufutwa kazi kwa lunga kiriri

jazanda uk.74,methali,kinaya ,ritifaa ,uk.69 kimopndo kwa lunga,misemo/nahau

Sura ya 6.

Mandhari: - shule ya Tangamano, darasani
- Kuna kurejelewa kwa msitu wa mamba
- Mji wa Karaha alikotorokea Umu unatajwa

Wahusika: - Umulkheri
- Mwalimu Dhahabu
- Naomi - mkewe Lunga Kiriri(mamake Umulkheri)
- Lunga Kiriri(babake Umulkheri)
- Sally
- Billy
- Sauna - kijakazi wa lunga
- Dick na mwaliko ndugu za umulkheri
- Hazina –mvulana wa mtaani
- Julida Uk.10

Matukio: - Umulkheri anasimulia shida alizopata baada ya babake kuaga na mamake kuwaacha.Uk.82
- Kijakazi Sauna anawatorosha nduguze – Umulkheri, Dick na Mwaliko.
- Umulkheri anahamia karaha na kusaidiwa na Hazina hadi Makao ya watoto.
- Wizara ya elimu inahamisha Ukmu hadi Tangamano.
- Mwalimu dhahabu anamsaidia umulkheri kwa mawaidha.

JB KIPSANG

Mbinu za lugha:- methali

- Barua (uk.71,72)
- Mbinu rejeshi – umu
- Hotuba ya Lunga –Uk 68-69
- Ritifaa Uk.69 – kimundo kwa Lunga
- Tasfida
- Jazanda, taswira, nahau/misemo.

Maudhui: - Ukiukaji wa haki za watoto kama utekaji nyara wa Sauna
- Ufisadi
- Usaliti – Naumi +Lunga
- Sauna anasaliti Dick +Mwaliko kwa kuwatorosha.

Sura ya 7.

Mandhari: - Shule ya Tangamano kwenye bweni la wanafunzi

Matukio: - Usimulizi wa;
- ✓ Kairu
- ✓ Umulkheri
- ✓ Mwanaheri (bintiye Kaizari na subira, dadake Ridhaa)
- ✓ Zohali 98 – alizaa – Nasibu(101)
- ✓ Chandachema – bintiye Fumba na Rehema. Uk.102-103

- Kairu
  - wanatoroka kwao baada ya fujo cha baada ya uchaguzi.
  - Anapoteza ndugu yake
  - Wanahamia kambini
  - Wazazi wanauza samaki(91/92)
- Mwanaheri
  - Mamake (Subira) alitoroka kwa kuwa na tofauti na mavyaa wake
  - Barua Uk 95-96 inaeleza sababu za kutoroka kwa subira.
- Zohali
  - Uk.98-100 alipata mimba akiwa mchanga akazaa Nasibu, wazazi matajiri wakamkataa
  - Anapelekwa kwenye kituo cha wakfu wa mama Paulina.
- Chandachema
  - Bintiye Fumba (mwalimu) na Rehema (mwanafunzi)
  - Analelewa na nyanya mzaa baba(Fumba)
  - Nyanya huyo anakufa mwanaheri akiwa darasa la 7

JB KIPSANG

- Fumba hakukubali kumlea chandachema, alihamia ng'ambo
- Chandachema alilelewa na majirani. Anaishi kijiji kilicho shamba la majani chai cha Tengenea.
- Alihamia shule ya kilimo - ya mwalimu mkuu Bi. Tamasha.
- Aliishi nyumbani mwa Tenge na Bi.Kimai.
- Tenge ni asherati
- Aliishia makao ya jeshi la wajane wa kristu. Uk 108.

Maudhui: - uwajibikaji
- Umuhimu wa familia katika malezi
- Elimu – kubadilisha mkondo wa maisha.

Lugha: - Taswira
- Methali
- Tashihisi
- Nahau/msemo
- Tashbihi
- Takriri
- Kinaya

Sura ya 8

Mandhari: - Nyumbani mwa Rachael Apondi na Mwangeka, karibu na kidumbi.

Matukio: - Mwangeka na Apondi wanawatazama Sophie, Ridhaa na Umulkheri wakiogelea.
- Kumbukumbu za Mwangeka zinahusu uchumba wake na Apondi Rachael.
- Rachael anatoa hotuba kuhusu amani na vyombo za usalama
- Mwangeka anavutiwa – wanachumbiana
- Rachael alikuwa mkewe Mandu aliyekufia nje akidumisha amani.
- Walijaliwa – Sophie
- Baadaye na Mwangeka walijaliwa Ridhaa.
- Wanamchukua Umulkheri na kumlea.

Maudhui: - Utu – uwajibikaji – Rachael Apondi Mwangeka kumlea Umu
- Amani – hotuba ya Rachael
- Umuhimu wa familia katika malezi(Uk 17)

Lugha: - Hotuba ya Rachael

JB KIPSANG

- Sitiari jazanda
- Tashbihi
- Maswali balagha
- Sadfa ya Rachel na mwangeka kuwa na maafa yanayofana na baadaye kupendana na kuoana

Sura ya 9.

Mandhari: - Dick na kijana mwajiri wake wamo katika uwanja wa ndege wanaelekea ng'ambo kununua vifaa vya simu.

Matukio: - Dick anaelekea ng'ambo kununua vifaa vya simu
- Anakumbuka biashara ya kuuza dawa za kulevya aliyoingizwa na Sauna aliyemuuza kwa (Buda).
- Anajiuliza waliko Umu na Mwaliko, nduguze
- Dick anaacha ulanguzi na kufanya usomi wa teknolojia ya mawasiliano ya simu na kujiajiri
- Umu yuko kwenye foleni pia, uwanja wa ndege anaenda ng'ambo kusomea shahada ya uhandisi katika kilimo.
- Jina Umu linamzindua Dick, wanakutana kisadfa.
- Dick alikumbuka (mbinu rejeshi) kisa Lemi na Tindi – alipofikiria kukataa kazi ya Buda ya kuuza dawa za kulevya.
- Lemi alipigwa mawe akafa kwa kusingiziwa wizi.(120-122)

Maudhui: - ukiukaji wa haki za watoto – Buda anatumia Dick kuuza dawa za kulevya.
- Ujenzi wa jamii mpya – Dick kuacha kuuza mihadarati
- Uozo – dawa za kulevya
- Uwajibikaji – Dick kujiajiri
- Mchango wa vijana – Dick kujiajiri, Umu kusoma hadi ng'ambo.

Wahusika: - Dick
- Umu
- Lemi(aliyeuawa kwa kusingiziwa wizi)
- Tindi (dadake Lemi)

Lugha: - Hadithi ndani ya hadithi
- Mbinu rejeshi
- Methali
- Kinaya
- Uzungumzi nafsia
- Sadfa – kukutana kwa Umu + Dick uwanja wa ndege.

Sura ya 10.

Mandhari: - Mtaa wa kazikeni – kwa Shamsi/Dengelua
- Mtaa wa Afueni – wanakoishi Ridhaa – matajiri wengine.

Matukio: - Wimbo wa shamsi/dengelua, mlevi unaangazia shida za maskini.
- Ridhaa anajenga kituo kipya cha Afya – mwanzo mpya.
- Anaajiri Selume na Kaizari.
- Humu wanahudumiwa wagonjwa kama –
  - Tuama_ anaponea kufa kutokana na tohara.
  - Pete – mkewe Fungo – aliavya mimba.
- Pete anateswa na Fungo kwa vile aliozwa kilazima kwake.
- Pete anaishia kuolewa na Nyangumi – anateswa na kuachwa.

Maudhui: - Ukengeushi – walioelimika wanakunywa pombe haramu na wengine kufa.
- Taasubi ya kiume – Fungo kutesa pete
- Elimu – kuchochea ukengeushi.
- Tamaduni potovu
  - Tohara – Tuama, ndoa za lazima
  - Kudhalilisha/kudharau wanawake – Fungu kudharau Pete.
- Utabaka
- Uongozi mbaya – Kituo cha afya cha uma kina ukosefu wa vifaa muhimu – Selume analalamikia.

Lugha : - Sadfa – Salome anataka wakati Kustaafu naye Ridhaa anafungua kituo kipya/cha afya hivyo kumwajiri.
- Tashihisi
- Majazi – afueni.fungo,nyangumi

Wahusika: shamshi /dengelua -mlevi

Bi. Halua-mkewe shamshi

Meko-mhudumu kituo cha afya cha mwanzo mpya

Selume - mhudumu kituo cha afya cha mwanzo mpya

Tuama:aiyenusurika kifo baada ya kutahiriwa

Kipanga :aliyenusurika kifo kutokana na pombe haramu

TAMIRA –dadake Tuama

Mzee maarifa:babake tuama

Pete- bibiye fungo na nyangumi-alinusurika kifo kwa kuavya mimba

Fungo :mumewe pete

JB KIPSANG

Nyangumi :mume wa pili wa pete

Patel :mwajiri wa Pete

Sura ya 11.

Mandhari:

Katika sura hii mandhari ni changamano:
- Mji wa **Ghushi** kwa Kangara.
- Sauna yumo huko.
- Nyumbani kwa Neema na Mwangemi
- Kituo cha watoto cha Benefactor, kwa mtawa Cizarina alikohifadhiwa Mwaliko baada ya kuokolewa na polisi mikononi mwa Kangara alipotekwa nyara na Sauna .

Wahusika

Mwaliko

Sauna – aliyerejelewa katika **uk.84 sura ya 6**. Mtekaji nyara wa Dick na Mwaliko.
- Neema (mkewe Mwangemi)
- Mwangemi(binamuye Mwangeka)
- Kangara – anayefanya biashara ya kuuza binadamu, amemwajiri Sauna.
- Mtawa Cizarina – msimamizi wa Benefactor – makao ya watoto.
- Bw. Maya – baba wa kambo wa Sauna – mbakaji
- Bw. Kero – baba halisi wa Sauna
- Mamake Sauna.
- Riziki immaculata .mtoto aliyeokotwa na Neema uk.163

Matukio:
- Sauna anahadithia maisha yake ya sasa kama mfanyakazi wa Kangara na mhusika katika ulanguzi wa watoto.
- Anasimulia maisha ya zamani namna aliishia kuwa katili – alibakwa na Maya(baba wa kambo) mama akafanya siri habari hiyo.
- Sauna alifanya kazi za kila aina baada ya kuteseka nyumbani;
  - ✓ Kwenye machimbo ya mawe
  - ✓ Ameuza pombe
  - ✓ Kuuza maji haramu(akilaghai kuwa ni mineral water uk.156)
  - ✓ Ulanguzi wa watoto ni **grassroot agent** uk. 157
- Anaishi mtaa wa Ghushi (uk.157)
- Sauna anapatikana na polisi akatiwa mbaroni na Kangara(uk.158)

- Mwaliko anaokolewa kutokana na utekaji nyara
- Mwaliko anapelekwa kitui cha Benefactor – kuendelea na masomo
- Maisha ya Neema na Mwangemi – Neema anapoteza watoto – mmoja kupitia sickle cell.
- Neema aliokota kitoto na baadaye kukipeleka kwa kituo cha Benefactor. Kiliitwa Riziki Immaculata (uk.163)
- Neema na Mwangemi wanaamua kumchukua Mwaliko kama mwanao
- Mwangemi anasomea chuo kikuu shahada ya Isimu na Lugha.

Maudhui:
- *Ukatili* – ulanguzi wa watoto, mihadarati
- *Ufisadi* – kuuzia watu maji ya kawaida kama mineral water.
- *Ukiukaji wa haki za watoto* – Sauna kutorosha Mwaliko na Dick kwa Kangara.
- *Ubakaji* – Maya – Sauna
- *Uwajibikaji* – Neema+ Mwangemi kulea Mwaliko, Cizarine kulea watoto wa benefactor.
- Unyanyasaji wa kijinsia(ubakaji)

Sura ya 12

Mandhari: - Hoteli ya majaliwa

Matukio:
- Ni siku ya kuzaliwa ka Umulkheri na Mwangemi
- Sadfa inakutanisha familia ya Umulkheri(aliyelelewa na Mwangeka) na Mwaliko aliyelelewa na Neema na Mwangemi.
- Wanakumbuka(Mwangemi na Mwangeka) maisha ya utotoni namna waliadhibiwa na Mwimo Msumbili(babu yao).
- Naomi anahadithia maisha ya mateso baada ya kumtoroka Lunga na kuhamia mjini kutafuta riziki, aliajiriwa na Kimbaumbau uk.191.
- Aliishia kufungua ofisi karibu na chuo kikuu cha Mbalamwezi awapigie wasomi kazi zao chapa. Uk 193

Maudhui:
- uwajibikaji
- Ujenzi wa jamii mpya
- Malezi

Mbinu za lugha:- sadfa
- Mbinu rejeshi
- Kuchanyanya na kuhamisha ndimi(uk.182,183,)

JB KIPSANG

- Taswira ,litifati uk.187 .kukariri maneno ya mwalimu wa dini
- Chuku.uk.181
- Methali

Wahusika: - Mwangemi
- Neema
- Mwangeka
- Umulkheri
- Dick
- Mwaliko
- Naomi
- Kimbaumbau

SURA	WAHUSIKA WAPYA WANAOIBULIWA
1	11
2	15
3	2
4	4
5	10
6	10
7	18
8	2
9	3
10	12
11	8
12	2
JUMLA	**97**

JB KIPSANG

JB KIPSANG